

HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'

SHULE YA SEKONDARI GANANA
S.L.P 235
KATESH.
1/12/2022
SIMU 0787886610

KUMB. NA. GNN/USL/VOL.I/2023

Jina la Mwanafunzi

Shule ya msingi alikotoka.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI GANANA WILAYA YA HANANG' MKOA WA MANYARA MWAKA 2023.

1.0. Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule yetu mwaka 2023. Shule ya Sekondari GANANA ipo umbali wa km 2 Mashariki mwa Mji wa Katesh Halmashauri ya wilaya ya hanang'.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 09/01/2023, unatakiwa kuwasili shuleni kuanzia tarehe 09/01/2023 na mwisho wa usajili ni tarehe 31/01/2023.

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. Sare za Shule

1. Wasichana

- i) Sketi mbili, urefu wa kutosha hadi kifundo cha chini cha mguu zenye rinda boksi na mfuko mmoja upande wa kulia.(**Aina ya kitambaa kimeambatanishwa kwenye fomu hii**)
- ii) Shati 2 blue bahari, aina ya tetroni mikono mifupi na vishikizo vya kawaida.
- iii) Soksi nyeupe ndefu(stockings) jozi 2.
- iv) Sweta la rangi ya blue bahari v-shaped

2. Kwa wasichana wa dini ya kiislamu, sare zinazokubalika ni hizi

- i) Sketi mbili, urefu wa kutosha hadi kifundo cha chini cha mguu zenye rinda boksi na mfuko mmoja upande wa kulia.(**Aina ya kitambaa kimeambatanishwa kwenye fomu hii**) AU
- ii) Kanzu 2 blue bahari ndefu mpaka magotini, pana na isiyo na mpasuo, mikono mirefu
- iii) Shungi 2 za blue bahari zisizo na urembo wowote zinazovuka viwiko vya mikono.

3. Wavulana

- i) Suruali 2 za blue bahari zenye rinda mbili na kunjo la “**turn up**” kwa chini, mfuko wa nyuma mmoja uwekwe kishikizo. Suruali iwe pana **inch 16 (isiwe mnyonyo)** na ndefu iguse kiatu.
- ii) Shati 2 blue bahari aina ya tetron, mikono mifupi na vishikizo vya kawaida.
- iii) Soksi za khaki jozi 2.
- iv) Mkanda wa suruali (mweusi) wenye chuma cha kawaida bila picha yoyote.
- v) Sweta la rangi ya blue bahari.

NB: Zingatia maelekezo juu ya mishono ya sare za shule. Zitakaguliwa ipasavyo.

2.2. Mahitaji ya jumla (wavulana na wasichana)

- i) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba za kufunga na visigino vifupi. Viatu visivyochongoka kwa mbele na bila muundo wa “Four angles”.
- ii) Tai mbili za rangi ya suruali/ sketi kwa wote isipokuwa kwa wasichana watakaovaa vazi la kiislamu tu.
- iii) Sweta lenye rangi ya blue bahari.
- iv) Sare za michezo kwa shule hii ni

Track suit ya rangi ya blue bahari.

2.3. Daftari kubwa 12, kalamu na mkebe wa hesabu.

2.4. Kamusi moja ya kiingereza ya oxford version.....

2.5. Gharama ya chakula cha wanafunzi kwa mwaka ni Tsh. 120,000/= na unaweza kulipa kwa awamu mbili (Tsh. 60,000/= kwa muhula) kupitia namba ya akaunti ya **NMB 41010006294** yenye jina la **“KAMATI YA CHAKULA GANANA SEKONDARI”**.

2.6. Mahitaji mengine ni:

- (i) (ii)

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu.

Kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo :-

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
- i) Kutunza mali za umma.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- a) Wizi.
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu mali ya umma.
- g) Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
- h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
- i) Kuoja au kuolewa.
- j) Kutoa mimba.
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- m) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

- a) Medical Examination form' ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

NB: Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA GANANA SKONDARI

.....
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI GANANA

FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

Mimi niliyechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Kwaraa kidato cha kwanza mwaka 2021. Nimesoma kwa makini na kuelewa maelekezo yote yaliyoandikwa hapo juu na nipo tayari kufuata kanuni, taratibu na sheria za shule na nitajituma kusoma kwa bidii, juhudi na maarifa kuhakikisha nafaulu kwa viwango vya juu na sitashiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.

Jina la mwanafunzi..... Sahihi..... Tarehe.....

Mtaa ninaoishi.....Kata ya..... Wilaya ya.....

SHULE YA SEKONDARI GANANA

KUKIRI KWA MZAZI/ MLEZI

Mimi..... (majina ya mzazi/mlezi) mzazi/ mlezi wa (majina ya mwanafunzi) aliyechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Kwaraa, kidato cha kwanza 2021, nimesoma kwa makini sheria, kanuni na maelekezo yaliyotolewa na shule na nimekubali kuyafuata, ninaahidi kufuatilia mwenendo wake wa kitaaluma na kinidhamu kwa kushirikiana na wanafunzi wengine, walimu na wadau mbalimbali wa Elimu.

Aidha nitamtimia mahitaji yake yote ya shule kwa wakati.

Jina la mzazi/ mlezi..... Sahihi.....Tarehe.....

Mtaa ninaoishi.....Kata yaWilaya ya.....

Namba ya simu ya mzazi/ mlezi namba hii iwe inapatikana kwa mawasiliano ya mzazi na uongozi wa shule.

MEDICAL EXAMINATION FORM

PART I:

(To be completed by Medical Officer in Mission / Government Hospital)

Student's full name..... Age: Date

- I.
 - a) Eye sight
 - b) Heart examination
 - c) Blood pressure:
 - d) Chest:
 - e) Hearing
 - f) Speech
 - g) Venereal diseases, Syphilis test
 - h) Leprosy
 - i) Sickle Cell test.....
 - j) Asthma
 - k) HB
 - l) Epilepsy
 - m) Skin Diseases etc
 - n) T.B Test
- II. Other serious diseases / Abnormalities

PART II:

I have examination the above named student and recommend that he/she is fit / unfit to join **GANANA SECONDARY SCHOOL**

Name of examiner

Designation

Station

Date

Sign: **Stamp:**